**"Yesu Kristo ni yeye yule Jana, Leo na Hata milelele"**

(Waebrania 13: 8)

# BARUA YA MUZUNGUKO NO. 23 OKTOBA 1980

Ninawasalimu wote kwa upendo katika Jina la damani la BWANA Yesu Kristo kupitia maneno ya Waebrania 13:20-21:

***"Mungu wa salama, ambae alimutowa kati ya wafu ule Muchungaji wa kondoo, kupitia damu ya agano la milele, Bwana wetu Yesu, awafanye wenye uwezo kwa kila tendo njema kwa ajili ya kutimiza mapenzi yake, na atende ndani yenu ambayo imupendezayo, kupitia Yesu Kristo, ambae kwake utukufu milelel na milele! Amen".***

Mungu ni Mungu wa salama, na wale alio wakombowa ni wana wa salama, imeandikwa:

***"Kwa maana Yeye ni salama yetu, Yeye ambae alifanya wawili kuwa mmoja na akaondowa ile ukuta wa matengano, uadui, ambae kupitia mwili wake akabomoa nguvu za ma agizo na matangazo yake, kusudi ndani yake aweze kuunda mtu mmoja mupya wale ambao walikuwa wawili, akirudisha salama, na kuwapatanisha mmoja na mwengine katika mwili mmoja pamoja na Mungu kupitia njia ya musalaba kwa kubomoa uadui."*** (Waefeso 2:14-16)

Hii siyo maneno ya bure ambayo haina maana, ila ni ukweli wa Kiunguambayo inapata zihirisho katika maisha ya wote walio kombolewa. Kupitia njia ya musalaba, uadui na ukuta ya matengano viliondolewa. Ile ambayo ilikuwa inatengenisha iliondoka ikaacha nafasi kwa ile ambayo inaunganisha. Andiko inamanishayale ambayo inasema. Mutu ambae amezaliwa upya ni mutu wa salama; kama mutu si wa salama, ni kusema ya kama hajafanywa upya. Mahali ambapo kweli kweli kazi ya ukombozi iliyomalizika inawekwa pembeni, na kisha ukuesabiwa haki kupitia njia ya sheria inalazimishwa, hapo ndipo uadui ya zamani inaleta mbegu mbaya. Sasa, kati ya wana wa Mungu ugomvi na ubishi; kupitia chuki inaamusha vita kwa namna ambayo haiwezi kuonekana ao kuifikiriwa kwa wale ambao wasiyoamini. Na sasa pale ambapo, kwa imani, kunakuwa pasipo kujizuiza kwa kazi ya ukombozi, hapo Yesu Kristo kama mutetezi anapinga mushitaka wa wandugu. Damu yake inafaa kwa kuunganisha, kusamehe na upatanisho. Watu ambao wamefanywa upya kindani mwao kwa wao wenyewe wanakuwa kweli wapatanishi. Sisi ambao tumepatanishwa na Mungu, tunaweza kujitukuza kwa neema iyoshinda hukumu. Swali la deni yetu imetiwa mara moja wazi. Kwa maana makosa yetu yote imewekwa juu yake; alichukuwa zambi zetu zote; na magonjwa yetu. Yeye

ni salama yetu na upatanisho wetu; ndaniya Mwokozi wetu kunapatikana wokovu na uponyaji kwa maana ni wokovu mukamilifu ambayo Mungu alitutolea katika Kristo. Ni Injili inayo dumu siku zote.

Wakati uadui ulikuwa ukifikia shabaa ya mwisho na wakati BWANA alikuwa akiondowa ukuta ya matengano, nguvu za giza zikafika kwa kushambulia, ushambulizi mukubwa juu ya mufalme wa salama. Kusalitiwa ambayo ilitumikishwa, ile hali ya kutolewa katika mikono ya wayuda, mashitaka, ile hukumu, ilekuhayarishwa ilimuleteya kuchukuliwa hata musalabani; aliteswakwa hayo yote bila kufungua kinywa, kama kondoo inayo pelekwa machinjoni. Ila hiyo haikukuwabado mwisho, kwa maana Mungu alikuwa akifuatilia lengo yake mukubwa ya mupango ya wokovu ambayo hata na wafasi wa Yesu hawangeweza kuelewa. Kulikuwa kumeonekana hali moja ambayo ilionyesha namna mambo ingelipashwa kufika. Ndipo sasa, kupitia ufufuko, maisha mapya ikaonekana kwa wale walio kufa katika Kristo na kufufuka pamoja nae. Maisha ya kiungu haiwezi kusimama sababu ya usaliti ao sababu ya kifo ya dunia. Ila maisha ya kiungu ilifunguliwa na ikaja kwa mbegu ya Mungu. Wana na binti za Mungu wana sehemu kwa mateso, kifo, ufufuko, kugeuzwa na kupanda kwa Yesu Kristo. Hakuna mutu ambae anaweza kushindisha mupango ya wokovu ambayo iliyo malizika katika Yesu Kristo. Tunasoma katika 1 Watesalonika 4:14:

***"Maanaikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao walio lala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye".***

Mungu ni Bwana juu ya maisha na juu ya kifo. Wale ambao wametoka katika mwili katika maisha ya hapa duniani, wanaendelea kuishi kwa Mungu katika hali ya roho. Kupitia damu ya agano la milele, Mungu wa salama alimuleta kutoka wafu Mufalme wa salama, Mufalme muchungaji mukubwa wa kondoo, ambae ni Bwana wetu Yesu Kristo. Roho wa Mungu, ambayo ni nguvu iletayo uzima, haingeweza kumufanya atoke kati ya wafu pasipo damu ya agano la milele kumwangwa kwanza. Na ni hivyo hivyo kwa wale ambao wanakubali zabihu ya kutolewa ya Yesu Kristo pamoja na imani itendayo kazi katika roho. Hatukusulubishwa tu pamoja na Bwana, tumefufuka vile vile pamoja nae kwa ajili ya maisha mapya na kupitia Yeye tunahesabiwa haki kwa hali kamilifu kwa utawa ya kazi ya ukombozi iliyo kamilishwa na Bwana Yesu Kristo. Mutume anaonyesha mawazo ya Mungu kutupatia mazuri yote ifaayo kwa kutimiza mapenzi yake. Ya muhimu katika ufalme wa Mungu, siyo kusema mapenzi ya mwanadamu ifanyike, ila tu mapenzi ya Mungu. Siyo kusema mupango yetu ikamilike, ila mupango ya Mungu iliyo pangwa nae tangu zamani. Ametujulisha mapenzi yake kupitia neno lake lililo funuliwa. Afanye atupatie nguvu ya kulitimiza. Ila inabidi yeye mwenyewe azalishe ndani yetu yale ambayo yana mupendeza. Ni hiyo ndiyo anaweza kutimiza

kupitia Roho ndani ya waliyo wake na kupitia hao ambao wataonekana mbele yake. Ndiyo sababu inatubidi tujiweke chini ya uongozi wa roho wake. Hiyo ikuwe ndiyo maombi ya imani yetuambayo inaingia mpaka kwa kiti cha enzi cha Mungu na ikubaliwe nae Mungu mwenyewe, ili atupatie yote ambayo ni mema kwa utimilifu ya mapenzi yake, na atende ndani yetu ambayo inayo mupendeza. Hapo sasa haitakuwa tena mutu, ila Mungu ndani ya Yesu Kristo ambae anapokea heshima ndani ya yote na kwa yote.

## WALINZI JUU YA KUTA ZA SAYUNI

Inayo husu matokeo ya kisiasa ya ulimwengu kufatana na Israeli, matokeo hiyo inastahili angalisho ya kipekee kwa upande wetu. Kwa jumla mutumishi wa Mungu hana huusiano wowote na kisiasa, hata hivyo hana huusiano pamoja na Umoja wa mazehebu hata na ma sehemu za kisiasa za kikristo za makundi mbalimbali. Kila mara wakati mutu anapewa kazi ya kiungu, hiyo inafanyikaka tu pasipo maamuzi ao mapenzi ya dini fulani, ila kila mara hiyo inahusu tu wale ambao wanayotenga sikiyo kwa ujumbe ya kiungu, ambayo inaletwa kwa kuambatana na neno ambalo Mungu alipana kupitia ufunuo wa ki unabii.

Ni jambo la nguvu sana tena lenye kutuhukumu, kwa kujuwa ni wakati gani, wapi na kwa mambo gani wito ya kiungu ilitolewa kwa mutumishi wa Mungu. Wote ambao wanaamini ujumbe ya nyakati za mwishowanashuhudia ya kama huduma ya ndugu Branham inahitajika kutambuliwa, kuheshimiwa, na ya kama ile ambayo alitangaza sawasawa na biblia inabidi iwekwe kwa matendo. Inabidi tena isemeke kwa wakati huu mmoja ya kama kuna alama na maana tofauti kwa ujumbe huu ambavyo haiwezekane kutiliwa kwa njia moja. Ndiyo sababu leo kuna ituna uwezo ya kujiitilia ndugu Branham, kama vile zamani watu walikuwa wakijiitilia Musa na Ibrahamu, na ijapokuwa hawako katika mapenzi ya Mungu.

Katika nyakati ngumu kama za leo, tuko na uwajibu mbele za Mungu kwa ajli ya taifa la Mugnu. Nyuma ya ndugu Branham kumaliza huduma yake, inatubidi tena kufanya mazoezi ya mwendeleo ya huduma hiyo. Na tena kwa uhakika ambao Bwana, kupitia kupuliziwa na roho, Bwana anasema leo kupitia maneno yote iliyo toka katika kinywa cha watumishi wake manabii na wamitume, tena kwa uhakika anatuzungumuzia hapo hapo kupitia mahubiri ya ndugu Branham ambazo zinaambatana na ushuhuda yote ya maandiko matakatifu. Inapo husu mambo ya ufalme wa Mungu, inatubidi kuambatana sana na kujiunga na kweli ya Mungu iliyo funuliwa na roho. Ila kwa kutimiza huduma inabidi ukuwe umeitwa na kuwekwa na Mungu yeye mwenyewe, pasipo hivyo tunaweka vizuizo kwa sisi wenyewe na kwa wengine, tukileta magonvi na mivurungano katika ufalme wa Mungu.

Hata hivyo na nabii Danieli (Dan. 9:1-3) alisoma katika nabii Yeremiya kwa kuchunguza na kutabuwa wakati ambao taifa la israeli ligeweza kurudi katika inchi yao vivyo hivyo nasi tugeweza kutafuta katika neno la unabii lililo funuliwa ilituweze kutambuwa niwakatigani ambayo tunaishi. Kama vile mikaya alileta ujumbe ya kiungu kwa Ahabu ikiambatana kikamilifu na unabii wa nabii Eliya, ndivyo hivyo shauku ya kilindini mwangu kuletea taifa la Mungu kwa kweli yotekwa yale inayohusika na wakati huu, na hiyo ni pamoja na uhusiano yote pamoja na manabii na wa wamitume, pia pamoja na ujumbe ambayo ndugu Branham aliyo leta kwa upande wa Mungu. Tunataka tuombe kikweli na kuamini ya kama Bwana yeye mwenyewe atafungua na kuangaza kwa mawazo yetu ya kiroho na kuelewa kwetu ili taifa la Mungu liweze kupewa muongozo wa kweli kwa saa inayofa. Kwa siku zetu haitoshe kupata jibu, ila kupokeya jibu inalotoka kwa Mungu.

## UNABII UNAKUWA UHAKIKA

Ndugu Branham alikuwa akisema: **"Ikiwa unataka kujuwa saa ya ya siku, angalia saa yako, ikiwa unataka kujuwa siku ya juma, angalia kalenda, ila ukitaka kujuwa ni saa gani Duniani, angalia kuIsraeli".** Mutu fulani alikuwa akitaja Israeli kama ni shindano ya zahabu ya saa ya Mungu. Ijapokuwa taifa hili linazarauliwa na kuteswa na dunia nzima, hauwezi pita karibu siku kabla ya siku kama haisemeke katika ma gazeti ao ndani ya taarifa ya ma habari. Katika juma hizi na katika myezi hii ya mwisho, mambo mengi imebadilika na tunaweza kuhesabu ya kama kwa muda kidogo watavumilia shida kwa shida na mambo yote ambayo itatimia.

Tukitaja Urusi kwa jina lake, siyo kwa sababu ya kisiasa ila ni kwa kweli na raisi kwa sababu inchi hii itakuwa na kazi ya kipekee ambayo ni ya maana kwa wakati ya mwisho katika unabii ya kibiblia. Kwanza katika mwaka wa 1933, Bwana akamwambia ndugu Branham: **„Fanya angalisho na Urusi! Fanya angalisho na Urusi, mfalme wa kaskazini!"**

Kama vile munavyo juwa, nilienda mimi mwenyewe huko Urusi, na ninaweza kusema ya kama hakuna kamwe taifa lingine hapa duniani ambalo linaweza kulinganishwa na taifa hili lenye kujishusha. Kulingana na ripoti nyingi sana, wakona maendeleo kuliko sisi. Ila hii inahusu mwendeleo ya historia ya wokovu, iliyo semeka tangu zamani katika biblia. Maandiko ya ki historia iliyo fanywa na watu inajiandika tena upya. Kwa hivi tena ndani yake kunasemeka historia ya wokovuiliyo andikwa na Mungu ambayo ni tofauti kwa jumla, iliandikwa tangu zamani katika wakati karibu myaka 7000. Matokeo yote iliwekwa tayari katika kitabo ya mwanzo mpaka kitabo cha ufunuo. Ni kwa namna hiyo ndiyo biblia inatofautiana na vingine vitabo vyote vinavyo kuwa duniani.

Mara na mara inayo husu Israeli na mataifa zingine zenye kuisumbua na kuishambulia, mioyo yetu inahuzunika. Hivyo hivyo tunapo fikiria nini mwisho ya maadui yake, ndani yetu, kwa uhakika hatufurahishwe na ile, ila tunaheshimu tu, na kwa heshima ya ndani, tunaheshimu mipango ya kiungu ya Mungu. Ni Bwana Mungu tu, ambae katika kujuwa kwake, aliweza kupanga vitu vyote tangu zamani kulingana na mipango ya mapenzi yake, ambayo kwa mwisho itatukuzwa na kuheshimiwa na ulimwengu yote, kila goti litagunjwa na kila luga watakiri; kwamba Yesu Kristo ni BWANA.

Mara nyingi katika maandiko matakatifu vitu haitajiwe kwa majina yao, ila tu vinapambwa. Haikuandikwaya kama mutu kwa jina la Yuda ndiye angesaliti Masia. Matokeo yaliweza tu kutangazwa pamoja na sehemu zao za kipekee na majina ikatajwa nyuma tu kwa wakati ya utimilifu wao. Ni hapo sasa, katika Matendo 1:16, ndipo Petro anatoa jina la msaliti kupitia maandiko akionyesha tukio ambalo roho mutakatifu alikuwa ametangaza mbele kupitia kinywa cha Daudi. Mpinga Kristo naye piyahatajwi kwa jina lake, anapambwa tu, na wote ambao wanaangaziwa na Roho Mtakatifu wanatambua, kulingana na maonyesho, ya kwamba huyu hawezi kupatikana katika dini ya kiyahudi, ao ndani ya ki islamu ao huko Urusi, ijapokuwa anaikala katika kikao kikuu cha kidini cha ulimwengu.

Katika Ezekieli sura ya 36 hadi 39 tunapewa mahusiano kati ya mfalme huyu wa kaskazini na taifa la Israeli walio kusanywa na kurudishwa katika nchi yake. Mara nyingikatika sura hizi ni swali la mtu huyu kutokamwisho wa kaskazini. Inazungumzwa juu ya Mufalme wa Roshi (sura ya 38) nakuhusu washirika wake, ambao wametajwa kwa jina lao kama kabila, tena imeandikwa: ***“...pande za mwisho za kaskazini, na vikosi vyake nvote, watu wengi pamoja nawe. Ujiweke tayari, namu, jiweke tayari, wewe na majeshi yako yote waliyo kukusanyikiya, nawe uwe jemadari wao!“*** (sura ya 38:6-7)

Jambo la linalo julikana muzuri ni kwamba Urusi haipatikane tu kaskazini, maana yake kaskazini mwa Israeli, lakini kwa "mwisho"kutoka kaskazini. Syria, Lebanonina Uturuki pia zinapatikana kaskazini ila hapana kwa mwisho ya kaskazini. Munatambua sasa jinsi maandiko matakatifu yanavyoeleza kwa usahihi nchi ambayo ndani yake kutatokea kiongozi ambaye atakusanyisha mataifa hayo mengi? Tunashangaa sana. Mungu alijua mambo yote kwa uhakika na anatupa maelezo ili katika wakati wa utimilifu tuweze kuyatambua. Upinzaniwa kweli waweza kushindwa wakati adui wa kawida anapatikana. Kuna muda kidogo na labda leotena, Uislamu unaona katika ukoministi sawa adui wake ya kifo. Kama vile Uislamu unavyodai kuwa ndiodini pekee duniani ambayo inaamini katika Mungu mmoja, na kwamba ni lazimaitetee imani hii na kuieneza kwa gharama yoyote na kwanamna wote, maana yake, hivyo hakika wakoministi wasioamini wanakanushauwepo wa Mungu – na bado

hizi kali mbili ambazo hazishirikiane kwa kitu chochote wanaungana dhidi ya taifa la Israeli watembelee juu yao. Ni Mungu wa Israeli ndiye aliyepanga mambo hivi ili hizi kauli mbili tofauti za ulimwengu, ile ya Uislamu na ile ya ukoministi, ziungane katika eneo ambalo Mungu alijifunua kwa zaidi ya manabii na ambapo sehemukubwa yahistoria ya wokovu tayari imepita, na itaendelea kutokea.

Kulingana na Zekaria 12:3, Yerusalemu ilipaswa kuwa jiwe mzigo kwa mataifa yote. Imeandikwa:

***"Tena itakuwa siku hiyo, nitafanyaYerusalemukuwa jiwe lakuwa lemeya watu wakabila zote, wote watakayo jitwika jiwe hilo wata pata jeraha nyingi, na mataifa yote ya dunia watakusanyika pamoja juyake."***

Hii inamaanisha ya kwamba mataifa yote, kwa sababu ya petroli, watalazimika kupiga magoti na kuwa adui kwa Israeli. Ila malazimisho zitatolewa siyo tu katika ndani ya uchumi, lakini pia kutoka kwa upande wa kijeshi. Taarifa rasmi, iliyochapishwa na shirika la vyombo vya habari la Soviet TASS inasema yakwamba Uturuki lazima iondoke kwenye mkataba wa Atlantiki (NATO), ilisababisha ikaonyesha kitu kikubwa ndani yangu. Kwa kufanya utafiti, niligundua kuwa Mesheki na Tubai, ambazo pia zimetajwa katika unabii wa Ezekieli, zilikuwa katika Uturuki ya leo. Tunaweza kuona hiyo kwenye taswira ya kijeografia za kibiblia. Kwa hivyo Uturuki, ambayo si mmoja wa ulimwengu wa Kiislamu, pia itainuka dhidi ya Israel.

Tangazo kwamba Syria itajiunga na mkataba ya Varsovia ilikuwa mshangao, lakini inafaa kabisa kwa jumla ya umoja. Huko Damascus ndio makao makuu ya OLP. Kwa hiyo jiji la Damascus litakuwa shabaa kuu ya mashambulizi kwa israeli. Nabii Isaya alisemakatika sura ya 17:1:

***"Tazama, Dameski umeondolewa usiwe muji, nao utakuwa chungu ya magofu."***

Ulimwengu wa ki arabu unaita wazi wazi kwa vita takatifu, hayo yote si kwa sababu eti ni vita ambayo imetiwa shurti na dini, ila ni kwa sababu imetajwa hivyo katika biblia. Sura 2 na ya 3 ya Yoeli ina ambatana na ile. Imeandikwa katika Yoeli 3:9:

***"Tangazeni haya kati ya mataifa, takaseni vita, waamsheni masuja, watu wavita nawakaribie, nawapande juu."***

Mambo haya yote hayatimilike machoni petu? Ikiwa tulikuwa hatufahamu ya kwamba Mungu iko kwa upande wa taifa lake Israeli lililo chaguliwa, nikwaoga tutakapo ona hayo yakitimia. Angalia mahali tunapo patikana kwa sasa: ulimwengu wa Kiarabu kwa jumla, adui mkubwa wa Israeli, ikiitwa kwavita takatifu. Watatafuta namna mupya yakufanya Misri kuwa adui ya Israeli, kwa kuwa hata na Etiopia itakamata sehemu

kwa vita na itapitia sudani na Misri kusudi kufikia Israeli; Libia itapigania Israeli, nayo itavukia Misri (Ezekieli 38:5).

Kwamipango ya kijeshi, Urusi imehakikisha nchini Syria uhuru kamili ya kutenda, uamuzi na namuna ya kutenda, inaweza kusonga mbele hata kufikia mpaka ya Israeli. Hii ina maana kwambamipango yote ya kivita inaweza kuchukuliwa kwa mikono yawataalamu bora wa kijeshi. Siku ya X (isiyo julikana), jemedari kichwa atatowa tu oda ya kusonga mbele wakati nae atakuwa amepewa oda kutoka juu, kwani imeandikwa:

***"Baada ya siku nyingi utakuwa kichwani mwao; nyuma ya myaka kazaa miaka utakwenda kupigana na nchi..."*** (Eze. 38:8)

***"Bwana MUNGU asema hivi; naam, siku hiyo watu wanguwa Israeli watakaa salama, utajua. Kwa hivyo utaiacha nchi yako, kutoka nchi za kaskazini, wewe na mataifa mengi pamoja nawe... Utasonga mbele dhidi ya taifa langu la Israeli, kama wingu likujalokufunika nchi. Katika siku zinazokuja, nitakufanya utembee juu ya nchi yangu..."*** (mstari 14-16)

***„Itakuwa katika siku za mwisho...“*** (Eze 38:16)

***"Nitakufundisha, nitakuongoza, nitakupandisha, nitakuweka juukutoka kaskazini, nami nitakuleta kwenye milima ya Israeli. Nitaangusha upinde wako kutoka mkono wako wa kushoto, nami nitaiangusha mishale yako kutoka mkononi mwako wa kuume. Utaanguka juu ya milima ya Israeli, wewe na majeshi yako yote, na mataifa yoteambayo itakuwa pamoja nawe; ndege wa kuwinda, kila chenye mabawa, na kwa wanyama wa porini nitakao wapa kuwa malisho".*** [Eze 39:2-4]

Tunaishi mwisho wa siku ambamo sehemu kubwa za ma unabii za kibiblia zinatimia mbele ya macho yetu. Mbele kwanza mashambulizi ya chuki yanaandaliwa dhidi ya Israeli, baadae ni ukingo wa kidini katika ulimwengu ya mupinga Kristokupiganisha kanisa la kweli la YesuKristo ambalo litakalo zihirishwa. Kama vile katika ulimwengu wa asili kunako ukoo kati ya uzao wa Israeli na ule wa Isaka, kwa hivyo katika uwanja wa kiroho kuna uhusiano kati ya ukriso ya kweli na ukristo ya uongo. Ni kwa sababu hiyo Ismaeli na Isaka wote walijidai kuwa uzao wa Ibrahimu kama baba yao, kwa kuwa alikuwa kweli baba yao. Wapinga Kristo na Wakristo wote wawili wanadai Mungu mmoja kuwa Baba. Ni lazima tulinganisheya asili na ya kiroho ili tuweze kupokea kwa jumla kuona na kupokea vile kuelewa wazi kwa kufuatilia mwendeleo ya mambo.

## MOTO KWA MIAKA SABA

Kulingana na Ezekieli 39:9 kazi ya kurudisha ya hiivita kubwa itachukua miaka saba. Itakuwa muda mrefu utakao tumikishwa kwa ku-

choma vyombo ya vita. Miaka saba itakuwa muhimu kuchoma vyombo vyote vinavyotumiwa kwa vita ambavyo vinaweza kuchomewa. Nivigumu kuaaminisha kuwa hii ndiyo vita ya mwisho ya Har-Magedoni ambayo, kulingana na Ufunuo 16, lazima ifanyike baada ya kikombe cha 6 chaghadhabu ya Mungu lazima kimwangwe juu ya dunia, yaani, nyuma ya kunyakuliwa kwa Kanisa, wakati wa dhiki kuu. Ni jambo ngumu isiyofikiriwa kwamba silaha zingeweza kuchomwa moto baada ya mwanzo wa milenia. Kwa hivyo haya yote yanapaswa kutokea mbele. Ndugu Branham alisisitiza kwa usahihi ukweli kwamba dunia ilipaswa kutayarishwa kupitia katika hatua tatu kwa ajili ya mileniamu. Alisema: **"Kwanza katika siku za Nuhu kulikuja ubatizo kwa njia ya maji ya gharika; pili, Yesu Kristo alimwanga Damu Yake katika dunia hii, ili kudai haki Zake kama Mumiliki wa asili juu ya waliokombolewa na hata juu ya hii dunia, tatu lazima kuwe na ubatizo wa moto, na utakaso lazima ukamilike kabla ya mileniamu kuanza."** Anaambatanisha hii na 2 Petro 3, na nyuma anaweka kilalo kati ya Ufunuo 21 na Isaya 65, anasema: **"Ilikuwa tu baada ya utakaso kwa moto kwamba Bwana kuweka miguu yake juu ya mulima wa mizeituni na nyuma anaingia katika Ubwana wake."** Muzozo ambao tulikuwa tukiuzingatia sasa hapa ulikaribia kwa njia wazi.

Hakuna mutu yeyote duniani anaye weza kujifanya mushauri mupendwawa Mungu, lakini kwa msaada wa Bwana tunachunguza matukio kupitia uongozi wa Roho Mtakatifu, na tutayaweka wazi kila mara kuambatana na maandiko matakatifu. Mwisho wa mambo yote umekaribia sana. Tunaweza tena kuongozwa upya na kujiachilia wenyewe tuongozwekuhusu musimamo ya mwisho ambayo inaleta maendeleo ya unabii. Marangapi tungeliweza kushukuru kwamba Mungu ametutumiya mtumishi wake na nabii, mpendwa wetu ndugu Branahm, naujumbe wa kinabii, ufunuo wa neno na njia za kiungu kwa ajili ya wokovu. Ni kwamambo hayo tumepokea ujumlawa matukio ya wakati wa mwisho.

## KUUNDA MAKUSANYIKO

Somo kuhusu kuanzishamakusanyiko mapya iliwekwa kwa oroza ya siku na watu wamoja, ambao bila shaka walikuwa na mafikiri mengine kuhusu somo hiyo. Daima kuna watu ambao wanakuwa nje ambao wangependa kujivunia kitufulani; wengine hata wanakuwa na haja ya manyoa za kondoo kuliko kondoo zenyewe. Mahali ambapo Roho Mtakatifu anafanya kazi kweli kweli, kusanyiko huwekwa bila hata watu fulani kulazimishwa kufanya safari kutoka nchi ya mbali na mzigo wakuunda makusanyiko. Wakati wa mitume, ndugu tofauti walitumika pamoja katika mahali mbalimbali, baadae wakaweka wazee. Mahali ambapo Roho wa Mungu anatenda kazi kweli kweli, hapo hakupatikane mabishano kuhusu jam-

bo moja ao lingine:wanatenda tu kulingana na Biblia. Mahali popote kunako inuka hapa na palemabishano isiyo na mwisho, jua kama sio Mungu anayeweka mkono Wake, ila watu. Kila mtumishi wa Mungu ana kusanyiko la mahali ambalo linakuwa kama ni nyumbani kwake. Hapa Krefeld, siku ya Jumamosi Fulani Bwana alinipa amri ya hapo hapo niweke ndugu wapendwa Russ na Schmidt kama wazee. Hii ikatimia kwa kukubaliana na kusanyiko lote, na hii ikafanyika kabla nianze huduma yangu ya kusafiri mahali pote.

Sasa hatuko mwanzoni ila mwishoni mwa wakati ya Ukristo. Haihusu mtu yeyote kujifanyia jina ili kwa mamulaka yake mwenyewe aweze kujiundia kusanyiko lamahali; Inabidi sasa kumutoa Bibi-arusi na kumutayarisha kwa ajili ya Bwana-arusi wake, nahili halipashwi kufanyika kwa namna ya mielekeo yote ya kidini ambayo tayari imeundwa. Ilibidi kwa shida, kwa hali ambayo ndugu Branham alikuwa anategemea kusanyiko moja tu ambalo angejivunia na kwamba kamwe katika myaka ya huduma yake hakuwai kuanzisha kusanyiko lingine. Ikiwa angefanya hivyo, angefuata nyayo za wale wote ambao ni waanzilishi wa makusanyiko, na kwa hiyo, angeweza kutiliwa shaka kwa huduma yake ya kiinabii. Wakati huu Bwana ametowa ujumbe wahapo hapo kwa watu wote wa Mungu, ambao wametapanywa katika mahali mbalimbali.

Ndugu Branham alipata maono ya kipekee; katika Roho akachukuliwa katika mbingu wazi na akaona karibu naye, kulia kwakena kushoto kwake, miti miwili ambayo ilikuwa ikibeba matunda mazuri zaidi. Sautiya Bwana ikasikilika kwake: **“Moja ya miti inamaanishawaamini wanaoshikamana na utatu, na mwigine unamaanisha wale ambao wanaambatanana Mungu Mmoja”.** Alipatikana kati yahiyo miti miwili, akaishika kwa mikono yake akaitikisa kwa nguvu zake zote. Matunda ikamwangukia kwa wingi. Maono haya hayahitaji mafasiriyo yeyote.

Hakuna sababu ya kubadili njia ambayo Mungu amechukua kwakipindi hikicha historia ya wokovu. Ni leokwamba ninaelewa kwa nini, wakati wa wito wangu, Bwana aliniambia: **“Usijishughulishe kwa kuunda makusanyiko na usitangaze kitabu chochote cha nyimbo”.** Ninasihi kila mmoja kuchunguza kama kazi hizizote zakidini hazionyeshi alamahizo hizo; Nikusemani alamaza kipekee za kizehebu.

Hata ziwe makanisa huru au ya kitaifa, makundi ao makusanyiko: Wote wameweka mafundisho ya imani yao chini ya makao makuu. Baadae, wakatangaza kitabo chao cha nyimbo cha kipekee ili kuleta mwelekeo mpya ya imani yao tofauti na wengine.

Hata hivyo, Bibi-arusi Neno siyo “chombo” ya dhehebufulani. Yeye ni zao la upendo wa Mwenyezi Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu, na amewekwa kando kwa ajili ya Bwana-arusi wa kiungu. Mara na mara ndugu Branham alisema hivi kwa uhakika: **“Katika uamusho huu**

**wa mwisho, hakutatokeya dhehebu jipya, bali kanisa Bibi-arusi".** Makusanyiko ya mahalini ni ya haki tena ni ya kibiblia; hata hivyo inaanza kamavile katika siku za kimitume, kwatendo la Roho. Kila kusanyiko la mahali limekabidhiwa kwa mzee ambaye anahudumu hapo, na ambaye Roho Mtakatifu amemuweka juu ya kundi la Mungu (Matendo 20:28). Sasa wakati tu wandugu kutoka inje watadhaniakujisikia kuwa na muzigo ya uangalinzi na kutawala juu ya makundi zingine, hiyo ni wakati ambayo ime chelewa. Hivyo ndivyo jinsi zehebu lakwanza la kikristo lilianza hapo Nikaea, natangu hapo ndipo wengine wote waliiga mfano wake. Hiyo ilinanza namna hii: Ndugu mmoja anajiwaziya kuwa nimtume au kitu fulani cha kipekee na anawakubalisha wengine; kwa hiyo wanakaa pamoja kujadiliana na kukamata maamuzi fulani ya kiakili na ya kibinadamu, ambayo hupambwa kuwa ya kiroho, na tayari hapo kitu cha kibinafsikinaanza – lakini ni Unikolai wa zamani ambao unatokea tena.

Tumeachiwa matendo ya mitume kwetu kama kielelezoisiyobadilika. Tulihubiri popote ambapo kulifunguliwa tu mulango mmoja: hekaluni, katika masinagogi, kwenye lango la Sulemani. Wale walio okoka walikusanyika upande mmoja na wengine ndani ya manyumba. Hapo ndipo walikuwa na ushirika katika sala, wakimega mkate na kufanya makutano yawatakatifu.

Ni ya kibiblia kweli kwamba iliyofanyika Zürich, kwenye nyumba ya taifa, mikutano ambamo watu wengi wanawezasikia Neno; na ni ya kibiblia kama katika mahali tofauti kuna mikutano ya maombi na matafakari. kila jambo kwa nafasi yake; lakini pia ni lazima tupate nafasi ambayo Mungu aliyoweka kwa ajili yetu. Kisha hapo tutakuwa na maisha ya haki katika shamba la kazi ya kanisa, na tutaheshimu agizo la Kiuungu.

Musi jiachilie kusumbuliwana mtu yeyote. Kulingana na Yuda 17-21, ni lazima kuwe na watu katika nyakati za mwisho ambao wataleta matengano na magawanyiko katika Ufalme waMungu. Inasemwa juu yaoya kwamba hawana Roho Mtakatifu, ijapo kuwa kwamba wanajiamini kuwa wao ni wa kiroho na kutembea kama hivyo. Hapa ndipo kunapatikana tatizo kubwa.

## AHADI YA UAMINIFU

Nakwa mwisho wa barua hii, ninawapa mazao ya ahadi na kiapo iliyoandikwa na kufanywa na waamini kwenye Maskani ya ndugu Branham. kama vile nilivyoipokea kuwa kama musaada kutoka ndugu Branham. Hakuna mwana memba hata mmoja alie jiandikisha, lakini alipenda kuwa na uhakika ya kwamba wale wote walio chukuwa maskani ya Branham huko Jeffersonville kama jamii yao ya nyumbani wasimame kikamilifu nyuma yake. Alitaka kujiepusha kusumbuliwa katika kazi ya huduma yake kutokea kwa wenye kutukana huduma yake ndani ya kundi lake,

matukano ambayo huleta matengano. Kwetu sisi, ni barua isioeleweka, lakini ni Bwana alie mwamuru hivyo. Ikiwa tunataka kuishi kukamilika kwa Kanisa na kupokea Baraka kamili za Mungu, inafaa masemi yote mabaya inakoma inayo kuwa kama kansa yenye kumaliza mwili, na kutumia wakati kwa kuomba. Mtu anayesimama kwa upande ya mtumishi wa Mungu ambaye aliitwa na kutumwa naye, mutu huyo anasimama kwa upendo wa Mungu:

## NUKUU YA HIYO BARUA

Ninatangaza wazi wazi kuunga mkono maskani ya Branham ambayo inaongozwa na muchungaji wake muheshimiwa William Branham, na kuunga mukono programu zake zote. Ninaahidi kutosema lolote mbaya dhidi ya ndugu Branham ama dhidi ya chochote cha programu zake, na mimi nitawakemea watakao ifanya. Nita mutii ndani ya haki na kosa, kamavileyeye mwenyewe anajibu kwa Mungu. Amina!"

## KAZI YA UMISHONARI

Kuna ripoti nyingi nzuri kutoka kwa kazi yetu ya umishonari. Safari yangu kupitia Ulaya Mashariki ilizidi matarajio yote. Furaha ilikuwa kubwa, ushirika wa karibu, baraka zilitiririka katika mito mikuu.


Mialiko huja kutoka duniani kote; hata telegramu zikiniomba nije. Tafadhali munikumbuke katika maombi yenu ya kila siku. Ninamshukuru kila mtu kwa moyo wangu wote ambaye anasimama nyuma ya kazi ya Mungu kwa njia yoyote . Kwa msaada wa Mungu, tutaendelea kutimiza ahadi ambazo tumefanya katika miaka michache iliyopita.

Katika tukio hili ningependa kuomba kwamba sisi sote tumwombee Dada Pilato na wamusika wake wawili. Baada ya kifo cha ndugu yetu mpendwa na mwenzetu mwaminifu Gino Pilati, wanahitaji utetezi wetu maalum. Tunataka pia kumpa Bwana kazi  ambayo inafanyika huko italiano.  Acha Bwana amjalie ndugu yetu malipo ya utumishi wake usio na ubinafsi na wa kujitolea siku hiyo.

Kwa hitaji ya wazi ya wazee wa kanisa, ningependa kuwapa ninyi salamu zao zote za uchangamfu katika umoja wa upendo wa kiungu.

Anae tenda kwa upande wa Mungu.

Ndugu Ewald Frank



Ikiwa unapendezwa kupokea vitabu vyetu,
waweza kutuandikia kupitia anwani ifwatayo:

Kituo cha Misheni Sanduku la Posta 100707 47707 Krefeld, Ujerumani

Waweza kuingia kwenye mtandao wakati wa mikutano yetu ya wikendi ya kwanza ya mwezi. Siku ya Jumamosi Jioni pa saa 19:30 h (Saa ya kati ya Ulaya), Jumapili asubuhi pa saa 10:00 h. Mikutano ya weza kusikilikana katika Lugha 13 tofauti duniani pote.

Pokeeni sehemu kwa yale ambayo Mungu anayo yafanya sasa kulingana na mpango wake wa okovu!

Ukurasa wa vuti: http://www. freie-volksmission. de

Barua pepe: volksmission@gmx. de

Fax: +49-2151/951293

or

Ukurasa wa vuti: www. misia. sk

Barua pepe: gospel2nations@misia. sk

Tel: +256 (0) 786 892 319, (0) 758 023 639, (0) 775 283 810

Na mwandishi na mchapishaji E. Frank